

**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM  
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS – MIVUMONI  
DAR ES SALAAM**

---

**MATANGAZO YA DOMINIKA YA 30**

**MWAKA C TAREHE 23 OCTOBA, 2022.**

**Kristo...**

**MCHANGO WA PILI**

Kwa ajili ya **UENEZAJI INJILI**. Jumuiya iandae vyombo, kwaya mtuongoze kwa wimbo.

**USHEMASI**

Shirika la Warosmini wanawatangaza kuwa Frateri Severine Onesphory Kilala, IC mzaliwa wa Moshi, Parokia teule ya Mt. Martin De Pores. Ni mtoto wa Onesphory Kilala na Aloicia Paul Tarimo.

Frateri Mathias Hamenyimana Misibo, IC mzaliwa wa Kaliua, Tabora, Parokia ya Mt. Anthony wa Padua mtoto wa Thomas Misibo na Agnes Chubwa.

Wanategemea kupewa daraja Takatifu la Ushemasi tarehe 16 Novemba 2022 katika Parokia ya Ekaristi Takatifu Lushoto.

Tuwaombe ili waweze kufika daraja hilo wanalolitamani.

**NDOA**

BW. Kalla Msigwa mtoto wa Meji Galamgendela na Fridah Urasa na Bi. Jesca Msheku mtoto wa Leons Stambuli na Bibiana Mwanamshiki.

**Tangazo la kwanza.**

Bw. Florence Furaha mtoto wa Laurent Temba na Gloria Salim na Bi. Agness Kalisa mtoto wa Kalisa Blasio Kyaruzi na Shelestina Kamanzi.

**Tangazo la Tatu na la mwisho.**

Anayejua kizuizi cha Tangazo hili atoe taarifa ofisi ya mapadre.

**UZINDUZI WA KWAYA YA MT. YOHANE PAULO WA II**

Kwaya ya Mt. Yohane Paul ii ya hapa Parokiani itafanya uzinduzi mkubwa wa Albam yake mpya iitwayo "Mwalimu wangu" iliyo katika mfumo wa video na audio, Leo .Uzinduzi utafanyika katika Misa ya kwanza na ya Pili.Waumini wote tunakaribishwa kuwaunga mkono katika kuinua kazi hii nzuri ya kumtangaza Kristu kwa njia ya uimbaji.

**UCHAGUZI**

Kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa kwaya za Mt.Maria de Mattias na Kristu Mfalme Leo tarehe 23/10/2022 na kwaya ya Mt. Yohane Paul II Dominika ya tarehe 30/10/2022 mara baada ya Misa ya kwanza.Wasimamizi wa uchaguzi ambao bado hawajachukua makabrasha ya uchaguzi wafike ofisi ya H/ walei kuchukua makabrasha hayo.

### **SHUKRANI**

Tunawashukuru wakristu wote waliojitokeza jana kwenye usafi wa makaburi, mahudhurio yalikuwa Zaidi ya watu 200 kwa makaburi yote mawili na sadaka ilikuya ni sh. 264,850 na itatumika kuomba misa za marehemu.

### **UJENZI**

Tunaendelea na kazi ya plasta eneo la nje ya jengo la ofisi kazi hiyo inategemewa kukamilia ndani ya mwezi huu.

### **HUDUMA KANISANI**

Leo tunahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Yohane 23 Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Josephine Bakhita Wakati huohuo Jumuiya ya Mt. Anthony wa Padua wajiandae

### **MAUZO**

Gazeti la Tumaini letu linapatikana kwenye duka la WAWATA kwa shilingi 1,000 tu. Jipatie nakala yako ilio sheheni habari kemkem.